

Kuishi Maisha Yanayompendeza Mungu (Sehemu ya 2)

Inategemea sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha Nini Hasa?* kinachopatikana kwenye jw.org/sw.

LENGO: Chunguza mambo unayoamini na sababu za kuamini mambo hayo, chunguza kile ambacho Biblia inafundisha, na uone jinsi unavyoweza kuwaeleza wengine mambo unayoamini.



JE, TUNaweza Kumpendeza Mungu Licha ya Mashambulizi ya Shetani?

1 CHUNGUZA MAMBO UNAYOAMINI

Kwa nini huenda watu wengine wakasema hapana?

Kwa nini huenda wengine wakasema ndiyo?

Wewe unaamini nini?

Kwa nini unaamini hivyo?

2

CHUNGUZA KILE AMBACHO BIBLIA INAFUNDISHA

Mwanamume mwaminifu Ayubu alifaulu kuvumilia mashambulizi ya Shetani.

(Ona sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 6-12.)

Soma Ayubu 1:10, 11.

Shetani alifanya nini ili kujaribu kuvunja urafiki wa Ayubu pamoja na Mungu?

Soma Ayubu 1:22; 27:5.

Ayubu aliitikiaje mashambulizi ya Shetani?



Mizizi ya mti inapokuwa yenye kina, ndivyo mti huo unavyoweza kustahimili dhoruba. Vivyo hivyo, kadiri urafiki wetu na Yehova unavyoimarika, ndivyo tutakavyofaulu kuvumilia magumu

Shetani anataka uache kumtumikia Yehova, lakini kwa msaada wa Yehova, unaweza kuvumilia.

(Ona sura ya 12 ya kitabu *Biblia Inafundisha*, fungu la 13-16.)

Soma Methali 24:10 na 1 Petro 5:8.

Tunajuaje kwamba Shetani hutumia mashambulizi ya moja kwa moja (kama mateso) au ya hila (kama kuvunjika moyo) kutufanya tupoteze urafiki wetu na Mungu?

Soma Ayubu 42:12-17 na Methali 27:11. (Tazama picha mwanzoni mwa makala hii.)

Tunajuaje kwamba Yehova anafurahi tunapodumisha uaminifu wetu kwake?

Unahisije kujua kwamba maamuzi unayofanya maishani yanaweza kufurahisha moyo wa Yehova?

3

ELEZA MAMBO UNAYOAMINI

MTU AKISEMA...

Ikiwa mtu anapatwa na magumu, hilo linamaanisha ametenda kosa fulani.

UNAWEZA KUSEMA HIVI...

Huenda watu wengi wanaamini hivyo. Lakini mimi siamini hivyo kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?

MTU AKISEMA...

Kwa kuwa Mungu ni Mweza Yote, matendo ya wanadamu hayamwathiri.

UNAWEZA KUMJIBU HIVI...

Ni kweli kwamba Mungu ni Mweza Yote. Lakini ninaamini kwamba *tunaweza* kumfurahisha, kwa sababu...

Utamsomea andiko gani?

Kwa kuzingatia maoni yake, unaweza kumsaidiaje kuelewa andiko hilo?
